## TAARIFA AMBAZO NWFHA INAHITAJI ILI KUWASILISHA MALALAMIKO YA HUD

1. Jina na anwani yako
2. Jina na anwani ya mtu/watu au shirika ambalo unawasilisha malalamiko dhidi yake
3. Anwani ya makazi yaliyohusika
4. Muhtasari wa taarifa ya kweli ambayo inaelezea hali ya ubaguzi
5. Tarehe ya/za ukiukaji unaoshukiwa.

## NINI KITATOKEA BAADA YA MALALAMIKO KUWASILISHWA HUD?

- Msajili wa HUD atayapitia malalamiko ili kubaini kama HUD ina mamlaka ya kufanya uchunguzi.
- Msajili anaweza kuomba taarifa za ziada, au kuhariri na kukuomba usaini upya malalamiko.
- Kama HUD imeyakubali malalamiko, ama mchunguzi wa HUD atapewa jukumu, au malalamiko yako yanaweza kupelekwa WSHRC ili wafanye uchunguzi.

## UCHUNGUZI:

Kwa kawaida mchunguzi wa HUD/WSHRC:

- wataratibu mahojiano yako ili kujua zaidi kuhusu malalamiko yako
- watamhoji Mshtakiwa
- watakuomba ushiriki katika mahojiano ya pili ili kujibu taarifa iliyotolewa na Mshtakiwa (kujibu hoja)
- watakuomba nyaraka (mfano, mkataba wa upangishaji, notisi, kumbukumbu za nyumba, simu, barua pepe, na kumbukumbu za ujumbe wa maneno, n.k.) taarifa za shahidi, na ushahidi mwingine kuhusu madai ya ubaguzi
- watakuomba utoe ushahidi kuhusu hasara uliyopata, ambayo inaweza kuwa ya fedha (kwa mfano, gharama za kuhama au ongezeko la kodi), majeraha ya mwilini, au mfadhaiko wa kihisia.

Uchunguzi utachukua muda. Tafadhali kuwa na subira na endelea kuwasiliana na NWFHA ili tuweze kukupa taarifa.

## MARIDHIANO

Wakati wa uchunguzi, HUD wanaweza kujaribu kuyashughulikia malalamiko kwa mkataba wa maandishi ambayo yanajumuisha masharti yoyote yaliyokubaliwa na wote wewe na Mshtakiwa. Makubaliano haya huitwa Mkataba wa Maridhiano au Mkataba wa Maafikiano ya Kabla ya Uamuzi. HUD haiamui kama ubaguzi ulifanyika na Mshtakiwa hakubali kosa lolote. Mlalamikaji hupokea chochote kilichokubaliwa. Faraja hii inaweza kujumuisha fidia ya fedha, vilevile makubaliano kutoka kwa Mshtakiwa ya kufanya mambo ambayo yatasaidia kuzuia ubaguzi wa siku zijazo, kama vile kupitisha uchunguzi unaotii Sheria ya Makazi ya Haki na sera zinazofaa za malazi, kuweka alama za makazi ya haki, na kupata mafunzo ya makazi ya haki.

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

## JE, MALALAMIKO YANAISHAJE?

Kama malalamiko hayatatatuliwa kwa mkataba wa usuluhishi, HUD itaamua kama Mlalamikaji amethibitisha ubaguzi huo. Kama sivyo, malalamiko yametupiliwa mbali kwa uamuzi wa "Kutokuwa na Sababu ya Msingi". Kama HUD itabaini kwamba ubaguzi umetokea, itatoa uamuzi wa “Sababu ya Msingi”, na kuyapeleka malalamiko kwenye Idara ya Sheria ya Marekani. Usikilizaji wa shauri wa utawala unaweza kuendeshwa mbele ya Hakimu wa Utawala, au mhusika yeyote anaweza kuamua kuwasilisha malalamiko hayo katika Mahakama ya serikali kuu badala yake. Idara ya Sheria (DOJ) haimwakilishi Mlalamikaji, lakini inaweza kupata fedha au ufumbuzi mwingine kwa ajili ya Mlalamikaji. Pia unaweza kumpata wakili wako mwenyewe ambaye anaweza kukuwakilisha katika kesi hiyo.

Kazi iliyotoa msingi wa chapisho hili iliwezeshwa kwa kiasi fulani na ufadhili wa Idara ya Makazi na Maendeleo ya Miji ya Marekani. NWFHA inawajibika kipekee kuhusu usahihi wa taarifa na tafsiri zilizomo katika chapisho hili.

Julai 2021 /Kiingereza—**SWAHILI**



# Jinsi ya Kuwasilisha Malalamiko ya Makazi ya Haki kwenye HUD

NORTHWEST FAIR HOUSING ALLIANCE

*“Inafanyakazi kuhakikisha makazi sawa kwa*

**(509)-325-2665**
**1-800-200-FAIR (3247)**
**www.nwfairhouse.org**

## UNALINDWA

Sheria ya Makazi ya Haki inakataza ubaguzi wa makazi kwa misingi ya *kabila, rangi, asili ya kitaifa, dini, jinsia* (ikiwemo *mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia*), *hali ya kifamilia* (watoto wenye umri chini ya miaka 18 katika kaya) na *ulemavu*

Aidha, Sheria ya Jimbo la Washington Inayopinga Ubaguzi (WLAD, RCW 49.60) inakataza ubaguzi wa makazi kwa misingi ya *hali ya kijeshi au ustaafu wa jeshi, imani, hali ya ndoa, mwelekeo wa kingono, na uhamiaji au hali ya uraia*

**Idara ya HUD (Makazi na Maendeleo ya Miji) ya Marekani** ni shirika la serikali kuu ambalo linatekeleza **Sheria ya Makazi ya Haki**

**Tume ya Haki za Binadamu ya Jimbo la WA** inatekeleza WLAD.

**Northwest Fair Housing Alliance** inaweza kukusaidia kuwasilisha malalamiko ya makai ya haki kwa HUD au WSHRC

Wasiliana Nasi Leo:

35 W. Main Ave., Suite 250
Spokane, WA 99201
Simu: (509)-325-2665 au
1-800-FAIR (3247)
FAKSI:-866-376-6308
www.nwfairhouse.org

**Tunaweza kukushauri kuhusu machaguo yako.**

## Je, ni jinsi gani Northwest Fair Housing Alliance Inasaidia?

Tunaweza kukusaidia kwa:

- Kubaini kama HUD, au WSHRC, zina mamlaka ya kupokea na kuchunguza malalamiko kuhusu kile kilichokukuta
- Kuhakiki na kuzipanga nyaraka au ushahidi ulio nao
- Kuandaa malalamiko ya kuyawasilisha kwa HUD
- Kutuma malalamiko kwenda HUD
- Kusimama kama mwakilishi wako wakati wa mchakato wa uchunguzi wa HUD
- Kukusaidia kuandaa ombi la uharibifu na masharti ya upatanisho kupitia mkataba wa usuluhishi

MUHIMU

***Northwest Fair Housing Alliance haitoi uwakilishi, ushauri wala huduma za kisheria.***
Malalamiko yaliyowasilishwa HUD yanachunguzwa kiutawala na shirika la serikali kuu; hayawasilishwi Mahakamani (ingawa, kama baada ya uchunguzi HUD itabaini kwamba ubaguzi ulifanyika, inaweza kuyapeleka malalamiko kwenye Idara ya Sheria ya Marekani, na upande wowote unaweza kuamua kuwasilisha kesi katika Mahakama ya serikali kuu).

Huna haja ya kutumia huduma za NWFHA kuwasilisha malalamiko kwa HUD. Unaweza kuwasiliana na HUD moja kwa moja:
*Simu: 1 (800) 669-9777 au*
Tovuti: https://www.hud.gov/program_offices/fair_housing_equal_opp/online-complaint

Sio lazima uwasilishe malalamiko kwa HUD. Badala yake unaweza kufungua kesi Mahakamani. Unaweza kutaka kushauriana na mwanasheria ili kuamua kama kuwasilisha malalamiko kwa HUD au kufungua kesi ndiyo njia bora zaidi kwako.

## NANI ANAWEZA KUWASILISHA MALALAMIKO?

***Mtu yeyote aliyedhulumiwa anaweza*** kuwasilisha malalamiko kwa HUD. Mtu aliyedhulumiwa ni yule ambaye anaamini kwamba ameathiriwa na ubaguzi, au yuko karibu kuathiriwa. Mtu anayewasilisha malalamiko ni “**Mlalamikaji**.”

## JE, UNAWEZA KUWASILISHA MALALAMIKO DHIDI YA NANI?

Mtu au shirika ambalo malalamiko yanawasilishwa dhidi yake hujulikana kama **“Mshtakiwa”.** Washtakiwa wanaweza kuwa wamiliki wa nyumba, wasimamizi wa nyumba na wafanyikazi wa matengenezo, waendelezaji, madalali wa nyumba, wakopeshaji wa rehani, vyama vya wamiliki na wamiliki ubia wa nyumba, mashirika ya bima, na wapangaji wengine au majirani wanaoingilia haki zako za makazi ya haki.

Baadhi ya watoa huduma za makazi ambao hawamiliki nyumba nyingi wamesamehewa kutii sheria za makazi ya haki. NWFHA inaza kukusaidia kujua kama mtoa huduma wako wa nyumba amesamehewa.

## JE, NI WAKATI GANI MALALAMIKO YANAWEZA KUWASILISHWA?

- **Mwaka mmoja (1) tokea** tarehe ya kitendo cha mwisho cha ubaguzi kinachoshukiwa ili kuwasilisha malalamiko ya kiutawala kwa HUD
- ***Miaka miwili (2) tokea*** tarehe ya kitendo cha mwisho cha ubaguzi kinachoshukiwa ili kufungua kesi ya madai katika mahakama ya serikali kuu au ya jimbo

## JE, INAGHARIMU FEDHA KUWASILISHA MALALAMIKO YA HUD?

Hapana. Hakuna ada kuwasilisha malalamiko ya makazi ya haki ya kiutawala kwa HUD.